STOF inavyochochea maendeleo katika sekta ya elimu mkoani Ruvuma

SAINT Teresa Orphans Foundation(STOF) ni Taasisi isiyokuwa na kiserikali iliyoanzishwa mwaka 2001 na inafanyakazi katika nchi mbili za Tanzania na Marekani.

STOF ilianzishwa awali kwa lengo la kusaidia watoto yatima na waishio kwenye mazingira magumu mkoani Ruvuma,kisha kuanzisha shule zake ili kusogeza huduma ya elimu kwa jamii wakiwemo watoto ambao walikuwa wanalelewa na STOF.

Tangu kuanzishwa kwa Taasisi hiyo watoto yatima zaidi ya 300 wamesomeshwa hadi vyuo vikuu ambapo baadhi yao wameajiriwa sehemu mbalimbali nchini na wengine wamejiajiri na kufanya shughuli zao binafsi

Mkurugenzi wa STOF nchini Marekani Teresa Nyirenda anazitaja shule ambazo zinamilikiwa na STOF kuwa ni pamoja na shule ya watoto wadogo ya Bright Future Hope iliyopo Mjimwema Manispaa ya Songea,shule ya Golden Gate International Primary School na Golden Gate secondary school zilizopo Seedfarm mjini Songea.

Akizungumzia shule ya watoto wadogo ya Bright Future Hope,Nyirenda anasema shule hiyo yenye hadhi ya kimataifa imekuwa kimbilia la watoto wadogo ambapo amesema STOF iliamua kuanzisha shule hiyo ili kuwafanya watoto wa Tanzania wanaosoma shule hiyo kuwa na mazingira sawa na watoto wanaosoma nchini Marekani.

“Bright Future Hope ni moja ya kitengo cha Taasisi ya STOF,hii ni shule ambayo inajaribu kumsaidia mtoto mdogo sio tu darasani,bali kwenye lishe ili wapate lishe bora,pia kumsaidia mtoto kuibua vipaji vyake vingine kama kuchora na muziki”,anasema Nyirenda.

Anasisitiza kuwa Bright Future Hope inaweka kipaumbele katika malezi ya mtoto kwa ujumla na kwamba ili kufanikisha lengo hilo STOF imeleta vifaa mbalimbali vya kissa kutoka nchini Marekani ambavyo Tanzania havipatikani ili watoto wa Tanzania nao wafaidike katika elimu.

Exvary Nkosi ni Mwalimu mwenye shahada ya Elimu ambaye anafundisha katika shule hiyo ya watoto wadogo anasema

amesomeshwa na STOF hadi elimu ya chuo kikuu ambapo ameamua kujitolea kufundisha katika shule hiyo ya chekechea inayomilikiwa na STOF.

Anasema licha ya kuwepo masomo ya mtaala wa kawaida, katika shule hiyo watoto hao wanajifunza uchoraji picha na kujifunza kutumia vifaa mbalimbali vya muziki ambapo anasema darasa moja linachukua hadi wanafunzi 30.

Kwa upande wake Cresensia Mbawala ambaye ni Mwalimu wa Bright Future hope anasisitiza kuwa kituo hicho ni cha kipekee ukilinganisha na vituo vingine vya kulelea watoto katika Mkoa wa Ruvuma.

Anayataja masomo wanayofundishwa watoto katika kituo hicho kuwa ni Hisabati,Kiswahili,Sayansi,Kiingereza na uchoraji na kwamba watoto wanapokea vizuri masomo hayo kutokana na kituo hicho kuwa na zana nyingi za kufundishia na kujifunzia.

Licha ya STOF kumiliki shule ya watoto wadogo ya Bright Future Hope,Taasisi hiyo pia inamiliki shule ya sekondari ya Golden Gate ambayo ni ya bweni iliyopo katika eneo la Seedfarm Manispaa ya Songea

Mkurugenzi wa STOF anasema kabla ya kuanzisha sekondari hiyo miaka ya nyuma watoto yatima ambao walikuwa wanalelewa na kituo hicho,walikuwa wanapelekwa kusoma katika sekondari zilizopo mbali na Songea na zilikuwa hazina mazingira bora ya kusomea na kuishi.

“Changamoto ambazo walikuwa wanazipata wale watoto,zilisababisha sisi STOF kujenga shule yetu ambayo imetatua changamoto hizo kwa kutoa elimu bora,chakula kizuri,mazingira bora ya kuishi na kusomea sanjari ya kuwa na walimu wenye viwango”,anasisitiza Nyirenda.

Anasema Sekondari ya Golden Gate inawaandaa watoto kama dhahabu kwa kulenga kufaulu vizuri na kuwa viongozi wazuri kuanzia ngazi ya familia kwa sababu wanaandaliwa kujitambua mapema tangu wakiwa kidato cha kwanza.

Hata hivyo anasema wamedhamiria mwanafunzi anayemaliza kidato cha nne katika sekondari hiyo awe sawa na dhahabu iliyosafishwa ndiyo maana sekondari hiyo inaitwa Golden Gate na kwamba wafanyakazi wote wakiwepo walimu wanafanya kazi ya ziada ili kuhakikisha wanatimiza malengo yaliyokusudiwa kwa ufanisi mkubwa.

Mkurugenzi huyo wa STOF anasema anajivunia kuwa na shule hiyo ambapo anasema kuna wakati utafikia kupata nafasi kwenye shule hiyo itakuwa changamoto kubwa kwa sababu mahitaji ya wazazi na walezi yataongezeka.

Anaitaja moja ya juhudi ya kuboresha elimu kwenye sekondari hiyo ni kuleta shehena kubwa ya vitabu toka ndani na nje ya nchi ambapo zaidi ya tani 12,000 za vitabu zimeletwa kwa mwaka jana pekee na kwamba chakula wanachokula wanafunzi ndicho wanakula walimu na watumishi wengine wa shule hiyo.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo Alberth Gama anaitaja sekondari hiyo ya kidato cha kwanza hadi cha nne inachukuwa wanafunzi wa kutwa na bweni na kwamba shule hiyo imesajiriwa mwaka 2003 na ilianza kuchukuwa wanafunzi wa kujiunga na sekondari mwaka 2004 hadi sasa.

Hata hivyo anasema sekondari ya Golden Gate inachukuwa wanafunzi mchanganyiko wavulana na wasichana ambapo inafanya vizuri katika matokeo ya kidato cha nne ambapo anaitaja siri ya kufanya vizuri ni utawala bora,walimu bora na wenye uzoefu wa kufundisha na kwamba mwalimu katika shule hiyo ofisini kwake ni darasani..

Anayataja matarajio ya baadaye ya sekondari ya Golden Gate kuwa ni kuwa na kidato cha tano hadi cha sita kwa mchepuo wa Sayansi na kwamba ujenzi wa majengo hayo umeanza.

“Shule hii ina kitengo cha ujasiriamali ambacho kinaitwa Beyond Academy,kinawawezesha wanafunzi katika muda wa ziada kujishughulisha na ushonaji wa aina mbalimbali hivyo wanapata ujuzi ambao utawasaidia kwenye maisha yao”,anasema Gama.

Moja ya malengo ya STOF ni kufungua na kusajiri shule mpya ya msingi ya kimataifa katika eneo la Unangwa Kata ya Seedfarm Manispaa ya Songea.

Meneja wa sekondari ya GoldenGate Moses Nyirenda anasema shule hiyo ya kimataifa ya msingi itaitwa Golden Gate Primary School ambayo inalenga kuwaandaa vizuri wanafunzi katika elimu ya msingi.

Anasema majengo ya shule hiyo yamekamilika ikiwemo madarasa na ofisi kwa viwango vya kimataifa ambapo STOF imekusudia kuwaandaa watoto kuanzia elimu ya chekechea,msingi na sekondari hivyo kuwa ukombozi katika elimu kwa watoto mkoani Ruvuma.

“Maandalizi ya kuifungua shule ya msingi ya kimataifa yamekamilika .hivi sasa tupo mbioni kuisajiri shule hii ili iweze kuanza kuchukua wanafunzi wa shule ya msingi”,anasisitiza Nyirenda.

Makala imeandikwa na Albano Midelo,ambaye pia ni Afisa Habari Mkoa wa Ruvuma